



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII



Simu Na: +255 - 272755016
Na: + 255 - 2753835
Tovuti: www.fiti.ac.tz
Barua Pepe: info@fiti.ac.tz

Chuo cha Viwanda vya Misitu
S. L. P. 1925,
Moshi.
Tarehe: 11/05/2017

TANGAZO

NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA YA VIWANDA VYA MISITU KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018.

Mkuu wa Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) - Moshi anatangaza nafasi za kujiunga na mafunzo ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu kwa mwaka wa masomo 2017/2018. Chuo kimesajiliwa na Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE) kwa namba REG/ANE/019.

A. Mafunzo yanayotangazwa.

- (i) Astashahada (Cheti) ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA- Level 4&5)
- (ii) Stashada (Diploma) ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA- 6)

B. Sifa za mwombaji.

- (i) **MAOMBI YA CHETI:** Awe amemaliza kidatao cha nne na awe amefaulu kwa alama D katika masomo MANNE (4) kati ya hayo, walau awe amefaulu kati ya masomo yafuatayo; Fizikia, Kemia, Biologia, Geografia, Hisabati na Kiingereza.
- (ii) **MAOMBI YA DIPLOMA:** Awe amemaliza kidato cha sita na awe amesoma michepuo ya sayansi na kufaulu walau somo moja kwa kiwango cha alama ya "D" au awe na cheti katika fani yoyote inayofanana.

C. Ada.

Ada ya mafunzo kwa mwaka ni sh. 800,000/= tu.

Wanafunzi wote wanajitegemea chakula na malazi wawapo chuoni, hata hivyo chuo kina nafasi chache za hostel ambapo kila mwanafunzi atakayepata nafasi hiyo atalipia sh. 270,000 kwa mwaka tu.

D. Jinsi ya kutuma maombi.

- (i) Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo atailipia shs 20,000/=
- (ii) Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi (form four leaving certificate, result slip/certificate, birth certificate) pamoja na nakala halisi ya slip ya benki.
- (iii) Fomu za maombi zinapatikana Chuo cha viwanda vya Misitu (FITI) - Moshi, kwenye Tovuti ya Chuo (www.fiti.ac.tz).

E. Tahadhari.

Mwombaji yeyote ambaye hatazingatia taratibu au mahitaji yaliyotajwa hapo juu maombi yake hayatafikiriwa. Aidha mwombaji atakayewasilisha vyeti na hati nyingine za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **20 August, 2017**. Maombi ambayo hayatapokelewa tarehe iliyotajwa hayatafikiriwa.

Maombi yote yatumwe kwa:

MKUU WA CHUO, CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU (FITI), S.L.P. 1925, MOSHI.

Kwa taarifa zaidi piga simu: **0752206305 au 0653027854**

IMETOLEWA NA: **MKUU WA CHUO- FITI**